JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI (TEAK) ILIYOPO MPAKANI KWENYE MISITU YA HIFADHI YA KWANI NA TONGWE WILAYANI MUHEZA NA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA NILO WILAYANI KOROGWE KWA NJIA YA MNADA

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)-Kanda ya Kaskazini unatarajia kuuza miti aina ya Misaji (tectona grandis (teak) yenye jumla ya meta za ujazo **1,600.883** iliyopo katika mipaka ya Misitu ya Hifadhi ya Kwani na Tongwe Wilayani Muheza na Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Nilo wilayani Korogwe. Jumla ya meta za ujazo **631.20, 602.89 na 366.703** zitauzwa katika Misitu ya hifadhi ya Tongwe, Kwani na Nilo. Miti hiyo itauzwa kwa mnada kwa kuzingatia kanuni ya 31 (ii) ya kanuni za Sheria ya Misitu za mwaka 2004. Miti hii ya Misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

MASHARTI YA MNADA

1. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mnada huu anatakiwa kuwasilisha maombi kwenye bahasha iliyofungwa kuonesha nia ya kushiriki mnada (rejea sehemu ya 14 ya Tangazo hili) akiambatisha leseni ya biashara, usajili wa kiwanda cha kuchakata magogo (2020/2021) au mkataba na mmiliki wa kiwanda cha kuchakata magogo (2020/2021) kwa asiye na kiwanda hicho, Usajili wa biashara ya mazao ya misitu 2020/2021) na nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Aidha, anatakiwa aoneshe jina la msitu ambapo miti hiyo ilipo na ujazo anaotarajia kununua kama ilivyo kwenye jedwali namba 1 hapo chini.

2. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi za **Misitu Wilaya ya Tanga** zilizopo **Chumbageni** jijini **Tanga** siku ya Ijumaa ya Tarehe **30/04/2021 saa 5:00 Asubuhi**. Mnada utafanyika kwa kufuata Sheria ya Misitu Sura 323

3. Miti hiyo katika kila eneo itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo, bei ya juu iliyotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.

4. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania- Kanda ya kaskazini unawaalika wanunuzi kutuma maombi yao kwa ajili ya kununua miti ya misaji kwa njia ya mnada ambapo mnunuzi anaweza kuchagua mojawapo kati maeneo yafuatavyo;

JEDWALI Na.1: ORODHA YA ENEO, UJAZO NA BEI

Na	**Jina la Eneo (Msitu)**	**Wilaya**	**LOT No.**	**Ujazo wa miti (m^3)**	**Bei ya awali kwa kila meta ya ujazo (TZS/M^3)**
1	Tongwe	MUHEZA	I	631.20	300,000
2	Kwani	MUHEZA	II	602.89	350,000
3	Nilo NR	KOROGWE	III	366.703	400,000
JUMLA				**1,600.883**	

5. Hati ya ushindi kwa mnunuzi aliyetaja kiwango cha juu kwa kila kiunga wakati wa mnada itatolewa.

6. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi isipokuwa baada ya kuchakata kwa mujibu wa kifungu cha 50 (1) cha kanuni za misitu za mwaka 2004 na Tangazo la Serikali Na.69 la Mwaka 2006..

7. Makampuni na watu binafsi wanakaribishwa kutembelea kukagua miti hiyo wakati wa siku za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri. Mhifadhi wa Misitu Wilaya/Mhifadhi Mazingira Asilia Nilo au msaidizi wake atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

8. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji wa miti ya misaji iliyopandwa kwenye mpaka wa msitu wa hifadhi ili kuepuka uharibifu wa misitu ya asili wakati wa uvunaji.

9. Bei ya kianzio kwa meta moja ya ujazo imeoneshwa katika Jedwali namba 1 hapo juu ikijumuisha ‘VAT’, ‘CESS’, ‘LMDA’, TaFF, Forest Royalty pamoja, na gharama za upandaji miti

10. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi baada ya mnada kufanyika. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mnunuzi atashindwa kulipa 75% iliyobaki. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yote yafanyike kwa kupitia mfumo wa makusanyo ya Serikali (MNRT PORTAL) baada ya kupewa Bill. Hati ya madai inayoonesha kiasi cha kulipa itatolewa na Mhifadhi wa Wilaya ya Muheza na Mhifadhi wa Mazingira Asilia Nilo. Malipo yanaweza kufanyika kupitia bank za NMB, CRDB, NBC, Bank ya Posta n.k

11. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa Mhifadhi wa Wilaya ya Mheza au Mhifadhi wa Mazingira Asilia Nilo kama uthibitisho wa malipo siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

12. Mnunuzi atakayeshinda ataingia mkataba na Wakala wa Huduma za Misitu wa kuvuna miti hiyo na kupatiwa leseni ya uvunaji siku 7 baada ya kukamilisha malipo yote kwa asilimia mia moja 100%.

13. Mteja atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya miezi miwili (siku sitini) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100.

14. Maombi yote yawasilishwe siku ya mauzo tarehe 30/04/2021 kabla ya saa 4:00 asubuhi katika ofisi ya Misitu Tanga Chumbageni jijini Tanga. Aidha, wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada

15. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mnunuzi yeyote atakayekiuka masharti ya mnada.

16. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za Wakala na Wizara: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz

limetolewa na

KAMISHNA MSAIDIZI WA UHIFADHI
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA-KANDA YA KASKAZINI
S.L.B 404
SAME - KILIMANJARO